

HABARI KITAIFA & KIMATAIFA

MAHAKAMANI

Stendi ya mabasi yazaa kesi ya dawa za kulevya

Na Kulwa Mzee

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi imewatia washtakiwa warne matatani baada ya kuwakuta na kesi ya kujibu, wakidaiwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine kilo 102 kutoka Stendi ya Mabasi ya Magufuli, Mbezi mkoani Dar es Salaam kwenda Tanga.

Uamuzi huo umetolewa na Jaji Godfrey Isaya, baada ya upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Erick Kamala kufunga ushahidi wao kwa mashahidi 10, na kueleza mahakama kuwa hawana shahidi mwingine zaidi.

Washtakiwa hao ni Maliki Maliki, Iddi Nassoro, Ally Jafari na Mwinyi Mgazija, ambao wanadaiwa kutenda kosa hilo Machi 24, 2022, katika eneo la Stendi ya Magufuli, Mbezi.

Akisoma uamuzi huo, Jaji Isaya alisema: "Baada ya kupitia ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, mahakama imejiridhisha kuwa washtakiwa wana kesi ya kujibu. Inawataka wote wajitetea."

Mara baada ya uamuzi huo, mawakili wa utetezi walieleza namna wateja wao watakavyojitetea.

Wakili Habibu Kassim, anayemtetea mshtakiwa wa kwanza, alidai mteja wake atajitetea mwenyewe chini ya kiapo.

Wakili Nehemiah Nkoko, anayewakilisha mshtakiwa wa pili na watatu, naye alidai wateja wake watajitetea kwa kiapo, huku wakitegemea ushahidi wao binafsi.

Wakili Wilson Ogunde, anayemtetea mshtakiwa wa nne, alidai mteja wake atatoa utetezi wake mwenyewe chini ya kiapo.

Mahakama imepanga kuanza kusikiliza utetezi wa washtakiwa hao tarehe 28 Oktoba mwaka huu.

Katika ushahidi uliowasilishwa na upande wa Jamhuri, Inspekta John Marwa alidai kuwa mshtakiwa wa kwanza, Maliki Maliki, ndiye mfanyabiashara mkuu wa dawa za kulevya, akiwagawia wenzake bidhaa hizo ili wauze.

Kwa mujibu wa Inspekta Marwa, Machi 24, 2022, akiwa na askari wenzake walifanya upekuzi katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli,

Mbezi na kuwakamata Ally Jafari, Maliki Maliki, na Iddi Nassoro Abdallah wakiwa ndani ya basi la kampuni ya Tashriff lililokuwa linakwenda Tanga.

Alidai kuwa wakati wa upekuzi, walikamata pochi nyeusi iliyokuwa na dawa za kulevya aina ya heroine, simu mbili, pamoja na tiketi mbili za safari.

Ilidaiwa mahakamani kuwa tiketi hizo zilikuwa na majina ya Ally Jafari na Saidi Saidi (jina linalodaiwa kutumiwa na Iddi Nassoro), zikionesha safari kutoka Dar es Salaam kwenda Tanga siku hiyo hiyo.

"Nilipewa jukumu la kuongoza uchunguzi wa shauri hili. Baada ya kukamilisha uchunguzi, tulibaini kuwa washtakiwa wote wanne wanahusishwa moja kwa moja na biashara ya dawa za kulevya," alidai Inspekta Marwa mbele ya mahakama.

Mahakama sasa inasubiri upande wa utetezi kuwasilisha ushahidi wao ili kutoa nafasi ya hukumu itakayobainisha hatima ya washtakiwa hao katika kesi nzito ya usafirishaji dawa za kulevya nchini.

ati ya changamoto iliyotajwa dhidi ya watendaji wa DART

Mchengerwa aelekeza DART, UDART kutatua changamoto mwendokasi Dar

Na MWANDISHI MAALUMU

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amekutana na viongozi wapya wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) na Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART).

Amewataka kutatua changamoto ya usafiri kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, kwani serikali imewezesha upatikanaji wa mabasi mapya.

Mchengerwa, alisema moja ya changamoto iliyokuwa ikikwamisha huduma ya usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam, ni matumizi ya lugha mbaya ya watumishi waliopewa dhamana ya kuwahudumia wananchi kupitia mabasi ya mwendokasi.

"Wananchi wengine wanakasirika tu kwa sababu ya lugha mbaya ya watendaji wetu wa mabasi ya mwendokasi, mtu amekaa masaa kadhaa kwenye kituo halafu matumizi ya lugha yanakuwa siyo mazuri, kwanini asikasirike."

Mchengerwa aliwataka viongozi hao

wapya kutoka ofisini na kwenda kufanya ufuatiliaji utakaobaini mienendo ya watumishi, inayosababisha kuibua kero na changamoto zinazokwamisha huduma ya usafiri kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam.

Aliwataka viongozi hao wa DART na UDART, kushirikiana kiutendaji, iwapo wanaona kuna changamoto zinazowakabili kiutendaji, wasisite kuwasiliana na Katibu Mkuu wa TAMISEMI, kuangalia namna bora ya kuzitatua.

Aliongeza baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kufanya mabadiliko ya uongozi wa DART na UDART, wananchi wamejenga imani, huduma ya usafiri itazidi kuboreka jijini Dar es Salaam.

Alitoa rai kwa viongozi hao, kuhakikisha wanailinda na kuiishi imani hiyo kwa vitendo.

Pamoja na hilo, Waziri Mchengerwa, aliwataka viongozi hao, kuhakikisha wanatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa Oktoba 02, mwaka huu jijini Dar es Salaam na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipofanya ziara ya kukagua hali ya utoaji huduma ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka kutoka Kivukoni hadi Kimara.

Aidha, Mchengerwa aliwataka

viongozi hao, kuhakikisha majaribio ya njia ya Mbagala, yanakamilika kwa wakati na wakamilishe mchakato wa kusaini mikataba ya wawekezaji, wakazi wa eneo hilo wapate huduma ya usafiri.

MWENYEKITI WA BODI

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART), Balozi Dk. Ramadhani Kitwana Dau, alimhakikishia Waziri Mchengerwa kuwa, viongozi wa UDART na DART, watatekeleza maelekezo aliyoyatoa kwa kufanya kazi kwa ushirikiano, kutatua changamoto ya usafiri jijini Dar es Salaam.

"Ninaamini ndani ya miezi sita, changamoto zote zilizokuwepo, zitabaki kuwa historia, ni kweli zipo, lakini zinatatulika ndani ya miezi mitatu.

"Kwa kiasi Fulani, tumeanza kupata pongezi ya maboresho ya huduma mara baada ya kuchukua hatua," alisisitiza Balozi Dau.

Katika kikao kazi hicho cha kuhimiza uwajibikaji, Waziri Mchengerwa, alifanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Bodi ya DART, David Kafulila na Mwenyekiti wa Bodi ya UDART Balozi, Dk. Ramadhan Dau na watendaji wakuu wa taasisi hizo.

TRANSPORT In line with its earlier announcement, the Second Phase operator officially began passenger trials along the Mbagala-Kilwa route at the weekend

BRT Phase 2 trial runs finally begin amid optimism, anxiety

The start of BRT services along the Mbagala-Kilwa corridor is set to complement, rather than replace, other modes of public transport used by thousands of commuters

By Gadosa Lamtey
@gadosa2
glamtey@tz.nationmedia.com

Dar es Salaam. If you thought the launch of Phase II of the Dar es Salaam bus rapid transit (BRT) would push minibuses, *bajajis* and motorcycles out of business, then you may need to think again.

The start of BRT services along the Mbagala-Kilwa corridor appears set to complement, rather than replace, other modes of public transport used by thousands of commuters travelling between the city centre and the densely populated Mbagala area.

Residents and operators of minibuses, *bajajis* and motorcycles who spoke to *The Citizen* yesterday described the launch as a "vital complement" to their businesses.

In line with its earlier announcement, the BRT officially began passenger trials along the Mbagala-Kilwa route at the weekend.

Chief government spokesperson Gerson Msigwa confirmed yesterday that the trial runs, conducted by Mofat Company, had started two days earlier and had now advanced to include passengers.

"The trials began on Saturday when the buses operated without passengers. Today they have started carrying passengers. We will continue in this phase while gradually increasing the number of buses on the route," he said.

Phase II of the BRT involves 250 buses operated by Mofat Company under a 12-year contract. All buses are powered by natural gas, aligning with the government's commitment to cleaner and more sustainable urban transport.

The launch of the Mbagala route



A BRT bus during trial runs on the Phase 2 route between Gerezaani and Mbalaga in Dar es Salaam yesterday. The trials began two years after the necessary infrastructure was completed. PHOTO | CORRESPONDENT

marks a major milestone in efforts to ease congestion and improve commuting efficiency in Dar es Salaam. Officials say the new BRT phase will significantly cut travel time between Mbagala and the city centre, offering a reliable and environmentally friendly alternative to conventional public transport.

However, local transport operators are optimistic that the new service will not edge them out of business. They believe demand for transport in Mbagala is simply too high for the BRT alone to handle.

Speaking to *The Citizen*, the treasurer of the Mbagala Rangi Tatu bodaboda station, Mr Said Khamis, said the system's launch

was long overdue.

"We don't see the BRT as competition. It has come to fill the gaps in public transport. Mbagala has many passengers and even after using the BRT, they still need to reach their homes. That's where we come in to complete the journey," he said.

Mbagala serves as a vital transport hub linking several wards within Temeke District including Mbagala Kuu, Chamazi, Charambe, Toangoma, Mianzini, Kiburugwa and Kijichi.

It is also a hub that links residents of Msongola and those as far as Zingiziwa and Chanika in Ilala District as well as those from

Mkuranga, Mwanedege, Vikindu and Vianzi wards in Mkuranga District, Coast Region.

"The BRT ends at Mbagala, so we'll still be required to ferry people to and from nearby areas. That means there's still plenty of business for us," he added.

A *bajaji* driver, Mr Shafii Mtiba, shared similar views, saying that while they may initially lose some long-distance passengers, new opportunities were opening up.

"In the mornings, we usually take many people to town, so that might change. But now we'll focus on local routes, taking passengers from BRT drop-off points to their homes. It's about working together

Trials began on Saturday when the buses operated without passengers

GERSON MSIGWA

to serve the people," he said.

Mr Khamis said that bodaboda riders were being reminded to observe traffic rules, particularly avoiding exclusive BRT lanes to ensure the system operates smoothly.

For a small trader and long-time Mbagala resident, Ms Shari-fa Yusuph, the BRT launch brings relief after years of unreliable transport. However, she cautioned against repeating past mistakes such as irregular schedules and long waits.

"Transport here has always been a major challenge, especially during peak hours. If the government is serious, this system should serve people reliably, not just become another political statement," she said.

Commuters who boarded the new BRT buses also expressed optimism mixed with concerns.

A resident of Mwanedege in Mkuranga District, Mr Juma Abdul said his trip from Mbagala to Gerezaani yesterday was impressive but noted operational issues.

"I waited almost an hour for the bus at Mbagala Rangi Tatu Station since only a few have been deployed so far," he said.

Abdul observed that some passengers queued for long periods to buy electronic payment cards needed for access to BRT stations.

"Many waited until the last minute because the launch had been postponed several times, so they were unsure it would really start. Some even paid others with cards to get access," Mr Abdul said.

With the services still new, several *bajajis* and motorcycles were still observed plying the BRT lanes as of yesterday, something that will have to cease as services proceed.

USAFIRI

Kauli za wananchi mwendokasi Mbagala 'ikitestiti mitambo'

Baraka Loshilaa, Mwananchi
bloshilaa@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Baada ya kuanza kwa majaribio ya Mabasi yaendayo Haraka (BRT) maarufu mwendokasi awamu ya pili Barabara ya Kilwa (Mbagala), madereva wa bajaji, pikipiki na daladala wamesema usafiri huo hautawaathiri huku abiria wakieleza matumaini pale utakipoanza rasmi.

Jana, madereva wa bajaji na bodaboda wameukaribisha usafiri huo wakisema baadhi yao wanaopakia abiria bila kukaa vituoni wataumia.

Walisema neema pekee wanayoiona ni kwa wale wanaokaa kwenye vituo rasmi vya kupakia abiria, wakieleza kuwa kuanza kwa mradi huo ni neema ya kupata abiria wanaposhuka vituoni. Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa aliambia Mwananchi kuwa, majaribio ya usafiri huo yalianza tangu Oktoba 10 mwaka huu huku ya jana yakihusisha uwepo wa abiria ndani ya mabasi hayo.

Kuanza kwa majaribio hayo kunahitimisha mlolongo wa ahadi kuhusu lini mradi huo upande wa Mbagala ungeanza, baada ya danadana za muda mrefu.

Danadana hizo zimeonekana baada ya Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka (Dart) Agosti 20, 2025 kutangaza kuwa, mabasi ya mwendokasi Barabara ya Kilwa yataanza safari Septemba mosi mwaka huu. Ahadi hiyo haikutekelezeka kama ilivyoahidiwa kwa kuwa, baadhi ya miundombinu haikukamilika hivyo siku rasmi ya kuanza huduma hiyo ikasogezwa hadi Septemba 15, 2025.

Msemaji wa Serikali Msigwa alisema jana kuwa, tayari majaribio yameanza.

"Majaribio yameanza tangu juzi (Jumatatu) na jana (Jumatumi) mabasi yalianza bila



abiria, leo Jumapili (jana) yameanza kupakia abiria, tutakwenda hivi wakati tunaendelea kuongeza mabasi kwenye njia hiyo," alisema.

Wananchi na matumaini

Dereva bodaboda kutoka Mbagala Rashid Kachona alisema ujio wa usafiri huo hautawaathiri kwa kuwa, abiria wengi wanapenda kutumia usafiri huo.

"Abiria wagari ni gari, kama ni bodaboda watatumia bodaboda, utakuta abiria yupo kwenye foleni lakini anasema hawezi kupanda bodaboda bora asubiri gari hilo hili.

"Kuanza kwa usafiri huu, kundi la bodaboda watakoathirika ni wale wanaopandisha watu wawili kwa mkupuo, kwa Sh2,000 kwa kila mtu, hao ndio hawatapata wateja, sisi tulioipo vituoni tunawasubiri abiria washuke kwenye hayo magari," alisema bodaboda huyo.

Said Khamis dereva bodaboda Mbagala, amesema ana furaha kuona usafiri huo ukianza kwa majaribio kwa kuwa, kero ya usafiri Mbagala ni kubwa.

Abiria waki-kata tiketi za mabasi ya mwendokasi katika Kituo cha Mbagala Rangi Tatu jijini Dar es Salaam jana. Picha na Said Khamis

"Hatuoni kama mabasi haya yatatunyang'anya abiria ya yanakuja kuondoa changamoto ya usafiri, kwa sababu abiria waliopo Mbagala ni wengi hata ujio wa mabasi haya changamoto bado haitaisha, tutashiriki ana kuondoa changamoto ya usafiri," alisema.

Pia, alisema bado wanaendelea kuwaelimisha madereva wenzao kutopita barabara inayotumiwa na mabasi hayo ili mradi huo ufanye kazi ya kuwahudumia wananchi bila vikwazo, kwa kuwa wengi wanateseka kupata usafiri.

Mbagala ni kitovu muhimu cha usafiri kinachounganisha kata kadhaa ndani ya Wilaya ya Temeke zikiwamo Mbagala kuu, Chanazi, Charambe, Toangoma, Mianzini, Kiburugwa na Kijichi.

Pia, ni kitovu kinachowaunganisha wakazi wa Msongola na wale wa maeneo ya mbali kama Zingiziwa na Chanika katika Wilaya ya Ilala, sambamba na wakazi wa Wilaya ya Mkuranga kutoka kata za Mwandege, Vikindu na Vianzi, mkoani Pwani.

"Kuanza kwa usafiri huu, kundi la bodaboda watakoathirika ni wale wanaopandisha watu wawili kwa mkupuo, kwa Sh2,000 kwa kila mtu, hao ndio hawatapata wateja."

Rashid Kachona

Dereva bajaji, Shafii Mtiba alisema pamoja na hofu ya kupoteza abiria, zipo fursa watazipata kuanza kwa kazi kwa mabasi hayo.

"Asubuhi huwa tunachukua watu wengi kuwapeleka mjini, kwa maana hiyo lazima kutakuwa na mabadiliko mradi huu ukianza, sasa tutaaangalia njia zingine za ndani kuwapeleka abiria ili sote tufanye kazi ya kuwasaidia wananchi," alisema.

Dereva wa daladala aliyejitambulisha kwa jina moja la Hans, alisema ujio wa mabasi hayo hautawaathiri kwa kuwa, bado daladala zinaweza kuwepo barabarani.

"Sisi tutaendelea kuwepo, watatusaidia hawa kupunguza wingi wa abiria, Mbagala ina watu wengi, mabasi yanahitajika mengi zaidi sio tatizo la kutatuliwa ndani ya muda mfupi, kunahitajika muda wa kutosha," alisema Hans.

Mfanyabishara wa eneo la Mbagala Rangi Tatu, Sharifa Yusuph alisema kuanza kwa mradi huo kutawapunguzia msongo wa mawazo wanaoupata kila wakiwaza usafiri.

"Ni hatua nzuri kuanza kwa mabasi hayo, kero yetu Mbagala ni usafiri; msongamano wa watu ni mkubwa na watu muda wote wanagombea daladala, tunapongezewa usafiri huo, kwetu wametupunguzia mzigo," alisema.

Lelya Shaban, mkazi wa Chanika akielezea ahueni yake kwa kuanza kwa usafiri huo, alisema utawaokolea

muda wananchi pamoja na fedha nyingi wanazotumia kuwahi kwenye vibarua vyao.

"Mbagala usipoamka alfajiri sana, huwezi kuwahi unakokwenda kama unahitajika mapema, foleni ni kubwa sana na wakati mwingine gari linaweza kuharibika katikati ya safari msiwe na pakupita.

"Mwendokasi kwetu tunaona kama mkombozi utatusaidia sana, wamachinga, mama lishe na kina mama wanaowahi kununua samaki feri alfajiri," alisema.

Mkazi wa Mwandege, Wilaya ya Mkuranga, Juma Abdul ambaye amepanda usafiri huo kwa majaribio alisema safari yake kutoka Mbagala hadi Gereza jana ilikuwa ya kuvutia, lakini kuna changamoto za kiutendaji amezibaini.

"Nilisubiri takriban saa moja katika Kituo cha Mbagala Rangi Tatu kwa kuwa mabasi yaliyotolewa bado ni machache," alisema.

Pia, Abdul alisema baadhi ya abiria walilazimika kusubiri kwa muda mrefu kwenye foleni kununua kadi za kielektroniki zinazotumika kuingia katika vituo vya BRT. "Wengi wao walichelewa kununua kadi hizo kwa kuwa, uzinduzi wa huduma ulikuwa umeahiriwa mara kadhaa, hivyo walikuwa na shaka kama kweli ingetokea. Wengine walilazimika kuwalipa waliokuwa na kadi ili waweze kuingia," alisema Abdul.

Hata hivyo, jana kwa kuwa huduma ilikuwa mpya, bajaji na pikipiki kadhaa zilionekana zikiendelea kutumia njia za BRT.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya
Songea
Kituo cha Mji Mji Mkoa Ruwama
Shauri Moyo No. 53/2025
Jina la Mdal: HERITAGE COITAGE
Jina la Mdal: POTIN DAVID KIVUYO
KITUWA SHAIRINI MDAWA
I Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Mada Katika
Mahakama za Mwanzo
KWA: POTIN DAVID KIVUYO
Kwa kuwa mda amelewa/wametele mada yake
yao kwamba
KUKAZA HUKUMU MADAI NO 53/2025 YA HERITAGE COITAGE
Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria binafiti katika
Mahakama hi Tarehe 17 Mwezi 10 mwaka
2025 saa 02:00 Asubuhi/mchana kwa majibu
wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya
kurkkipa shauri hili ni lazima kuleta shahidi
madhidi wako na vielezo wote vinavyohitaji
shauri hili kwa ajili ya kujitegemea
ANGALIZO Kama hautohudhuria siku iliyotajwa
hapa juu, na ikihitajika kuwa upokea hata ya
kutawia chauri, Mahakama Rawareta husikiliza
shauri bila ya wewe kuwepo
Hali hi imetolewa kwa Amri na Mhakimu wa Mahakama
hii tarehe 10 mwezi 10 Mwaka 2025.